JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO

**BODI YA KOROSHO TANZANIA**

# TAARIFA KWA UMMA

## KUSITISHWA KWA KONGAMANO NA MAONESHO YA 19 YA MWAKA YA AFRICAN CASHEW ALLIANCE (ACA)

Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) inapenda kuutaarifu umma, wadau wa mnyororo wa thamani wa tasnia ya korosho, pamoja na washiriki wote waliosajiliwa na wale waliotarajia kujisajili, kwamba Bodi ya Wakurugenzi ya **African Cashew Alliance (ACA)** imetangaza kusitisha kwa muda usiojulikana **Kongamano na Maonesho ya 19 ya Mwaka ya ACA**, ambayo awali yalipangwa kufanyika kuanzia tarehe **18 hadi 21 Novemba 2025** katika Ukumbi wa **Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC)** jijini Dar es Salaam, Tanzania.

ACA imewahakikishia washiriki wote waliosajiliwa pamoja na waoneshaji kuwa **malipo yote yaliyofanyika yatahamishiwa na kutumika katika kongamano lijalo** litakalofanyika nchini **Ghana mwezi Septemba 2026**. Aidha, kwa washiriki wanaotaka kurejeshewa fedha zao, **maombi yao yatashughulikiwa kwa haraka na kwa uwazi.**

Bodi ya Korosho Tanzania inapenda kutoa **shukrani za dhati** kwa ushirikiano, uvumilivu na uelewa mliouonesha katika kipindi hiki. Tunaendelea kushirikiana kwa karibu na ACA kuhakikisha kwamba kongamano lijalo litafanyika kwa mafanikio, katika mazingira yenye **usalama, utulivu na uhakika.**

Kwa maelezo zaidi au maombi ya kurejeshewa fedha, tafadhali wasiliana kupitia barua pepe: **aca@africancashewalliance.com**

**IMETOLEWA NA:**

**MKURUGENZI MKUU**
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**
**8 Novemba 2025**